# Mapokezi ya Kisemantiki ya Nomino za Mkopo katika Kiswahili: Mifano kutoka Nomino zenye Asili ya Kiingereza na Kiarabu

Musa Mohamed Salim Shembilu

**Ikisiri**

Nomino za mkopo zinapoingia katika lugha kopaji huwa zinachakatwa katika viwango mbalimbali vya kiisimu. Nomino hizo zinaweza kuchakatwa katika kiwango cha kifonolojia, kimofolojia au kisemantiki. Michakato hiyo hutokea wakati wa kuzipokea nomino hizo ili kuzifanya ziendane na mfumo wa lugha kopaji. Lengo la makala hii ni kuchunguza namna nomino za mkopo zinavyopokewa kisemantiki katika Kiswahili. Je, nomino hizo zimepokewa na maana zake zote kama zilivyo katika lugha kopwaji au zimefanyiwa marekebisho yoyote? Kama zimefanyiwa marekebisho wakati wa kupokewa katika Kiswahili ni marekebisho gani hayo? Je, maana za nomino hizo zimepanuliwa, zimepunguzwa au zimegeuzwa? Vilevile, makala hii inachunguza sababu za mabadiliko ya maana zinazojitokeza wakati wa kupokewa kwa nomino za mkopo katika Kiswahili. Makala hii inaongozwa na Nadharia ya Sarufi Amilifu (*Functional Grammar Theory*) inayosisitiza kuwa mabadiliko ya maana ya maneno huukiliwa na matumizi ya maneno hayo na mahitaji ya mawasiliano ya jamii. Hivyo, mabadiliko ya maana yaliyotokea katika nomino za mkopo katika Kiswahili yanatokana na namna jamii ya Waswahili[1] wanavyozitumia nomino hizo au kutokana na mahitaji yao ya kimawasiliano**.** Makala hii inatarajiwa kuwa na manufaa katika taaluma ya semantiki kwa kuweka bayana namna nomino zinavyochakatwa kisemantiki na sababu ya kuchakatwa huko.

## 1.0 Utangulizi

Tunapochunguza namna nomino za mkopo zilivyopokewa katika Kiswahili, hatuna budi kuelezea japo kwa muhtasari muwasala wa jamii za lugha kopwaji na lugha kopaji. Kwa vile nomino za mkopo zinazotumiwa katika makala hii ni zile zenye asili ya Kiarabu na Kiingereza, hatuna budi kuzungumzia kwa ufupi muwasala uliopo baina ya Waswahili na jamii ya Waarabu na Waingereza. Waarabu[2] walianza kufanya muwasala na wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki katika karne za mwanzoni kabisa (Polomé, 1967; Nurse na Spear, 1985; na Lodhi, 2000). Kwanza kabisa walianza na muwasala wa kibiashara, ambapo walileta nguo, zana za chuma na shanga na wao walichukua dhahabu, mbao na watumwa. Kwa mujibu wa Nurse na Spear (1985), Waarabu hao walikuwa wakija kila mwaka kwa kutumia Pepo za Kaskazini za ‘Monsoon’.

Mara baada ya kufanya biashara kwa muda mrefu katika eneo hili, Waarabu walivutiwa na biashara hiyo na kutaka kulitawala eneo hili. Nurse na Spear (1985) wanadai kuwa mwishoni mwa karne ya 17 sultani wa Oman aliwafurusha Wareno katika maeneo ya Waswahili katika pwani ya Afrika

---

[1] Waswahili kwa mujibu wa makala hii ni wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki wanaozungumza Kiswahili kama lugha yao ya mawasiliano.

[2] Waarabu kwa mujibu wa makala hii ni wageni wote waliotoka Ghuba ya Urabuni (Arabian Gulf) ambao ni Waomani, Washirazi n.k.

Mashariki na kuanzisha utawala wake huko Zanzibar. Kuwapo kwa utawala wa sultani katika pwani ya Afrika Mashariki kulisababisha kuongezeka kwa mtagusano wa Waarabu na Waswahili (Ajayi, 1999). Muwasala huu wa Waarabu na Waswahili ulisababisha Kiswahili kisiepuke kuathiriwa na Kiarabu katika viwango mbalimbali. Mathalani, katika kiwango cha kifonolojia, Kiswahili kimekopa sauti za Kiarabu kama vile ث /***th***/, ذ /***dh***/, غ /***gh***/ na خ /***kh***/ ambazo zinatumika katika Kiswahili na kuonekana kama zina asili na lugha hiyo.

Vilevile, Kiswahili kinaonekana kuathiriwa sana kimsamiati na Kiarabu kutokana na kupokea maneno mengi kutoka lugha hiyo (Bosha, 1994; Lodhi, 2000). Nurse na Spear (1985) wanadai kuwa Kiswahili kina zaidi ya asilimia 50 ya maneno yenye asili ya Kiarabu katika nyanja za sheria, biashara, dini, mimea asilia na shughuli za uvuvi. Dai hilo limetiliwa mkazo na Lodhi (2000) aliposisitiza kuwa Kiarabu kinaongoza kwa kuchangia msamiati katika Kiswahili hasa katika fani za biashara, fasihi, dini na sheria. Kumekuwapo na tofauti za kiidadi katika nomino za mkopo katika Kiswahili. Hali hii inasababishwa na kila mtafiti kutumia vyanzo tofauti vya data. Mathalani, Zawawi (1979) alitumia Kamusi ya *Swahili – English Dictionary* (Johnson, 1939) na kubainisha kuwa kati ya maneno 3006 yasio ya Kibantu yanayopatikana katika kamusi hiyo, 80% yana asili ya Kiarabu. Mohamed (2010) naye kwa kutumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu (KKS)[3] anadai kuwa kuna jumla ya asilimia 19 ya maneno yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili. Japokuwa suala la idadi ya nomino za Kiarabu katika Kiswahili limekuwa na mvutano mkubwa lakini jambo ambalo wanaisimu wanakubaliana pasipo shaka ni kuwa Kiswahili kimekopa maneno katika Kiarabu.

Waingereza pia walikuwa na muwasala na watu wa Afrika Mashariki tangu miaka ya 1880. Katika miaka hiyo, kulikuwa na Waingereza waliokuwa wakifanya kazi pamoja na utawala wa sultani. Miongoni mwao ni Bw. John Kirk aliyekuwa mshauri mkuu wa sultani Barghash bin Said na Lloyd Methew aliyekuwa kamanda wa jeshi la sultani huko Zanzibar. Muwasala wa kiutawala kati ya Waingereza na jamii ya Waswahili, hasa wa Tanganyika na Zanzibar ulifanyika mara baada ya Vita Kuu vya Kwanza vya Dunia ambavyo vilitokea kati ya mwaka 1914 na 1918 (Parpart na Rostgaard, 2006).

Massamba na wenzake (2001) wanadai kuwa katika wakoloni waliopata kutawala eneo hili la Afrika Mashariki, Waingereza walifanya juhudi kubwa katika kukikuza na kukieneza Kiswahili. Katika utawala wa Waingereza ndipo lahaja ya Kiunguja iliposanifiwa na kupatikana kwa Kiswahili sanifu tunachotumia leo hii (Mbaabu, 2007 na Maganga, 2008).

Hivyo basi, muwasala huu wa Waingereza na Waswahili wa Afrika Mashariki, umesababisha Kiingereza kuathiri Kiswahili katika viwango mbalimbali vya kisarufi kama vile, fonolojia na msamiati. Athari hizo, hususani za

---

[3] KKS Toleo la Pili.

kifonolojia, zimesababisha baadhi ya mkururo wa sauti za Kiingereza kupatikana katika Kiswahili. Mathalani, katika Kiswahili kuna mkururo wa sauti kama vile *skr* katika neno *skrubu* ambalo linatokana na neno la Kiingereza ‘screw’ , *skw* katika neno *skwea* linalotokana na neno ‘square’ na *dr* katika neno *haidroliki* linalotokana na neno ‘hydrolic’. Kwa hakika mkururo huo wa *skr, skw* na *dr* haupatikani katika maneno yenye asili ya Kibantu isipokuwa umeingia katika Kiswahili kutoka katika Kiingereza. Pamoja na Kiswahili kuathiriwa sana na Kiingereza, hata hivyo, Kiswahili nacho kimekiathiri Kiingereza kimsamiati. Mathalani, Kiingereza kimekopa maneno kama vile *panga, shamba, safari* na *mzee* (taz. Kamusi ya *Oxford Advanced Learners’ Dictionary* (Toleo la 8)).

Kama tulivyoona kuwa Kiswahili kimeazima msamiati kutoka katika lugha za Kiarabu na Kiingereza, hivyo, ni dhahiri kuwa msamiati huo ulikuwa na matumizi au maana yake katika lugha kopwaji. Makala hii inachunguza ni kwa jinsi gani msamiati huo, hususan nomino zilivyopokewa kisemantiki katika Kiswahili. Lengo likiwa ni kuangalia kama nomino hizo ziliazimwa na maana zake zote au zilifanyiwa marekebisho. Katika kufikia lengo hilo, makala hii imegawanywa katika sehemu nne ambazo ni utangulizi, mapokezi ya kisemantiki ya nomino za mkopo, sababu za mapokezi hayo, na hitimisho. Data ya makala hii imetokana na utafiti uliofanywa maktabani kwa kutumia kamusi na vitabu vingine na uwandani katika mikoa ya Dar es Salaam na Mjini Magharibi huko Zanzibar. Watoa taarifa katika eneo hilo walipewa hojaji na kujaza na wengine walisailiwa kuhusu mapokezi ya kisemantiki ya nomino za mkopo katika Kiswahili. Uchambuzi wa data hizo uliongozwa na Nadharia ya Sarufi Amilifu iliyoasisiwa na Dik (1997). Nadharia hii inasisitiza kuwa vipengele mbalimbali vya lugha havishughulikiwi kwa kuangalia muundo wa vipengele hivyo pekee bali hushughulikiwa kwa kuangalia matumizi ya vipengele hivyo na mahitaji ya kimawasiliano waliyonayo watumia lugha husika. Mabadiliko ya maana yanayotokea pindi nomino za mkopo zinapopokewa katika lugha kopaji bila shaka hutokana na matumizi ya nomino hizo na mahitaji ya Waswahili katika kuwasiliana. Sehemu inayofuata tunaonesha ni kwa namna gani nomino za mkopo zimepokewa kisemantiki katika Kiswahili.

## 2.0 Mapokezi ya Kisemantiki ya baadhi ya Nomino za Mkopo katika Kiswahili

Nomino za mkopo zinapopokewa katika lugha kopaji zinaweza kuchakatwa kifonolojia, kimofolojia, kisemantiki na hata kisintaksia. Makala hii inachunguza namna nomino za mkopo kutoka Kiingereza na Kiarabu zilivyopokewa kisemantiki katika Kiswahili. Hivyo, tunaangalia nomino hizo za mkopo kama zilivyokopwa kwenda Kiswahili zilifanyiwa marekebisho yoyote ya kimaana au zilikopwa na maana zake zote katika Kiswahili.

Endapo nomino au maneno ya mkopo yamepokewa kwa kufanyiwa mabadiliko ya kimaana katika lugha yoyote basi ni lazima moja kati ya michakato mikuu ya kisemantiki ifuatayo utokee: Mchakato Panuzi wa Kisemantiki (Kuanzia sasa MPK), Mchakato Finyazi wa Kisemantiki (MFK), Mchakato Geuzi wa Kisemantiki (MGK) na Mchakato Kapa wa Kisemantiki (MKK) (taz. Whitney, 1867; Ullmann, 1977; Crowley, 1997; Campbell, 2004 na Narrog, 2012).

MPK ni mchakato unaotokea wakati nomino inapoongezewa maana ambazo hazikuwamo katika nomino hiyo kabla haijakopwa. Mathalani, nomino inaweza kuwa na idadi chache au mawanda finyu katika lugha kopwaji, lakini inapoingia katika lugha kopaji ikaongezewa idadi ya maana au ikapanuliwa mawanda yake. MFK nao ni mchakato ambao hufanya kazi ya kupunguza idadi au mawanda ya maana za asili zinazopatikana katika lugha kopwaji. Nomino ya mkopo katika lugha kopwaji huwa na maana nyingi au pana kimawanda lakini inapoingia katika lugha kopaji, maana hufinywa kiidadi na kimawanda. Mchakato wa MGK hutokea wakati maana za asili za nomino zinapobadilishwa kabisa na nomino hizo kupewa maana mpya katika lugha kopaji. Ikitokea nomino ya mkopo ikaingia na maana zake zote kama zilivyotumika katika lugha kopwaji, basi mchakato wa MKK hutokea.

Pamoja na michakato hiyo minne tuliyoijadili hapo juu, pia kuna michakato mingine midogo ambayo inaweza kutokea wakati nomino zikifanyiwa mabadiliko ya maana. Michakato hiyo ni Mchakato Ngonoshaji wa Kisemantiki (Kuanzia sasa MNK), Mchakato Sitiari wa Kisemantiki (MSK), Mchakato Pacha wa Kisemantiki (MPaK[4]) na Mchakato Metonimia wa Kisemantiki (MMK).

MNK ni mchakato ambao huichakata nomino kwa kuipa dhana ya ngono ambayo hapo awali haikuwapo. Kuna baadhi ya nomino maana zake ni za kawaida hazina dhana ya utusitusi lakini kutokana na mahitaji ya kimawasiliano ya lugha kopaji husababisha nomino hizo zikapewa dhana ya utusitusi. Mchakato mwingine mdogo ni MSK, mchakato huu hutokea wakati maana ya nomino inapobadilika kutokana na matumizi ya kisitiari. Matumizi hayo ya sitiari husababisha maana ya nomino kupanuka kwa kuhusianisha maana mpya na maana ya asili. MPaK hutokea kwa kupachuliwa au kugawanywa mara mbili kwa maana ya asili na kupatikana maana nyingine mpya. Kupachuliwa kwa maana ya asili ya nomino kunasababisha maana mpya kuwa na uhusiano na maana ya asili. MMK ni mchakato ambao kwa kiasi fulani unafanana na MPaK, lakini MMK huwa maana mpya haipachuliwi kutokana na maana ya asili, isipokuwa maana mpya nayo huwa na uhusiano na maana ya asili. Michakato hii midogo ni kama wakala tu wa michakato mikuu kwani kwa vyovyote itakavyochakata neno au nomino, maana za nomino hiyo zitaongezeka, kupungua au kubadilika kabisa.

---

[4] Tumeweka ‘a’ katika kifupisho hicho ili kutofautisha na mchakato wa MPK uliopo.

Baada ya kuifafanua michakato ya kisemantiki inavyoweza kutokea kwa ujumla hapo juu, katika sehemu inayofuata tunaonesha kwa mifano namna michakato hiyo inavyotumika katika kupokea nomino za mkopo katika Kiswahili. Katika kuonesha hilo, tumetumia mifano miwili miwili kwa kila mchakato mkuu.

### 2.1.1 Mifano ya Nomino za Mkopo Zilizopokewa kwa Kutumia MPK

Kama tulivyoeleza hapo juu kuwa MPK ni mchakato ambao nomino ya mkopo iliyokuwa na maana chache katika lugha kopwaji huongezewa idadi au mawanda katika lugha kopaji. Katika mchakato huu tumetumia mifano ya nomino mbili; moja kutoka Kiingereza na nyingine kutoka Kiarabu. Kutoka katika Kiingereza tumetumia nomino *goli* (*goal*) na kutoka Kiarabu tumetumia nomino *tajiri* ( تاج ). Nomino *goli* imechakatwa kwa kutumia MPK, japokuwa ndani yake kuna michakato mingine midogomidogo iliyochangia neno hilo lipanuliwe maana[5] zake katika Kiswahili. Michakato hiyo ni Mchakato Pacha wa Kisemantiki (MPaK), Mchakato wa Sitiari wa Kisemantiki (MSK) na Mchakato wa Ngonoshaji Kisemantiki (MNK). MPaK, MSK na MNK kwa pamoja imesababisha neno *goli* kupanuliwa maana zake. Neno hili (goli) katika Kiingereza lina maana[6] zipatazo nne (4) ambazo ni: 1. *Fremu yenye nyavu ambayo wachezaji lazima waingize mpira hapo wapate ushindi,* 2. *Kitendo cha kutumbukiza mpira golini*, 3. *Lengo, matarajio* na 4. *Sehemu inayoonesha mwisho wa mbio*[7]. Maana namba 1 na 2 ndizo zilizokopwa katika Kiswahili na kuachwa maana namba 3 na 4. Maana namba 1 (*Fremu yenye nyavu ambayo wachezaji lazima waingize mpira hapo wapate ushindi*) ilipokopwa katika Kiswahili ilichakatwa kwanza kwa kutumia MPaK, ambapo maana hiyo ilipachuliwa na kuwa mbili katika Kiswahili. Maana ya kwanza ni (*Mlango ulio katikati ya milingoti miwili katika mpira*) na ya pili (*Pete iliyotundikwa juu ambayo mpira hutumbukizwa*).

Tumebaini kuwa katika Kiswahili maana hizi mbili zinatokana na maana moja inayohusu sehemu ambayo mpira huingia. Maana namba 4 (*Nafasi ya konda katika basi*) na namba 5 (*Sehemu ya kupatia riziki kama vile duka n.k*) katika Kiswahili zimepatikana kwa kuchakatwa kwa maana namba moja (1) kwa kutumia MSK. Maana hizo zimefananisha kisitiari kati ya goli la uwanjani na mlango wa basi ambapo konda husimama kama golikipa na kuchukua nauli na sehemu ya biashara ambapo mfanyabiasha husubiri wateja awahudumie. Aidha, maana namba

---

[5] Maana za mifano ya nomino zilizotumika katika makala hii zinatokana na kamusi (Tazama katika marejeo) mbalimbali na utafiti alioufanya mwandishi kuhusu matumizi ya nomino hizo katika jamii ya watumia Kiswahili.

[6] Maana hizi zimetafsiriwa na mwandishi kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili.

[7] Mfano maana hizi zinapatikana katika *Oxford Advanced Learners' Dictionary* (Toleo la 8) na kamusi nyingine za Kiingereza.

mbili[8] katika Kiingereza imekopwa kama ilivyo na kuingia katika Kiswahili. Hata hivyo, maana hiyo imengonoshwa kwa kuchakatwa kwa kutumia MNK ambapo maana hiyo (*Kitendo cha kutumbukiza mpira golini*) imelinganishwa na mwanamume anavyofikia kileleni katika tendo la ndoa hivyo ikatupatia maana ya 6 katika Kiswahili (*Kitendo cha kufika kileleni katika tendo la ndoa*).

Vilevile, nomino *tajiri* imechakatwa kwa kutumia MPK wa kiidadi na kimawanda. Nomino hiyo katika Kiarabu ina maana[9] moja tu ambayo ni *mfanyabiashara mweye duka.* Maana hiyo katika Kiswahili ilipanuliwa kwanza kimawanda na kuwa *mwenye mali*. Kutoka mfanyabiashara wa duka kuwa mtu yeyote mwenye mali; hapa mawanda ya maana hiyo yamepanuliwa zaidi. Baada ya hapo nomino hii ikapanuliwa kwa MPK kiidadi kwa kuongezewa maana mbili zaidi ambazo ni *mwajiri* na *mtu mwenye utoshelevu wa jambo fulani*. Kutokana na kupanuliwa kwa maana moja ya nomino *tajiri* iliyokuwapo katika Kiarabu, kwa sasa nomino hiyo ina maana tatu katika Kiswahili ambazo ni: 1. *Mwenye mali*, 2. *Mwajiri* na 3. *Mwenye utoshelevu wa jambo fulani.*

### 2.1.2 Mifano ya Nomino za Mkopo Zilizopokewa kwa Kutumia MFK

MFK ni mchakato ambao unaifanya nomino ya mkopo kupunguza maana zake zilizokuwa zikitumika katika lugha kopwaji kiidadi au kimawanda (Narrog, 2012). Katika mchakato huu tumetumia mifano miwili ya nomino zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu pia. Nomino hizo ni *bomu* (bomb) kwa upande wa Kiingereza na *taharuki* ( تحرك ) kwa upande wa Kiarabu. Nomino *bomu* katika Kiingereza ina maana 11. Maana za nomino hiyo *bomu* katika Kiingereza ni: 1. *Chombo kilicho na vitu visababishavyo mlipuko*, 2. *Kufeli*, 3. *Kushambulia kwa kutupa bomu*, 4. *Kwenda kwa kasi sana*, 5. *Kufanikiwa sana*, 6. *Pesa nyingi*, 7. *Atomiki* (*bomu*), 8. *Gimba la lava ngumu linalotupwa kutoka katika volkano*, 9. *Sigara yenye madawa ya kulevya*, 10. *Shambulio la bomu*, na 11. *Kutoa mtu katika nyumba kwa kutumia bomu*. Tukichunguza maana hizo za neno *bomu* inaonekana kuwa zinatawaliwa na dhana ya kitu kiletacho madhara. Maana zilizoonekana kubeba dhana nyingine ni namba 5 na 6 ambazo ni mafanikio na kuwa na pesa nyingi.

Nomino hii ilipoingia katika Kiswahili ilichakatwa kisemantiki na kubakiwa na maana nane ambazo ni: 1. *Silaha iliyotengenezwa na vitu vya mlipuko*, 2. *Kombora dogo*, 3. *Swali au fumbo gumu*, 4. *Ngoma; yenye sauti nzito, au sauti yake kubwa au namna ya kuicheza hapo zamani*, 5. *Mtu mwenye uwezo mdogo*, 6. *Jambo linalotarajiwa kuleta madhara baadaye*, 7. *Isiyofaa au hafifu iliyoghushiwa* na 8. *Danganya ili kupata kitu.* Kwa kulinganisha maana zilizomo katika Kiingereza na zile za Kiswahili ni maana mbili tu, yaani namba 1 na 2 ndizo

---

[8] Maana hii ndiyo imekuwa namba 3 katika Kiswahili baada ya kuingia kama ilivyo.
[9] Maana katika Kiarabu zimetafsiriwa na mwandishi kwenda katika Kiswahili.

zilizotoka katika Kiingereza baada ya kuchakatwa kwa MFK. Baada ya maana hizo mbili kuingia katika Kiswahili, kilichofanyika ni kupanua maana hizo kwa kufananisha madhara, umbo au matokeo ya silaha yenye mlipuko. Mathalani, fumbo gumu hufananishwa na bomu kutokana na madhara yanayoweza kutokea kwa mtu kama vile kuumbuka endapo atashindwa kufumbua fumbo hilo. Ngoma yenye sauti nzito imetokana na kufananishwa na sauti ya mlipuko wa bomu na jambo lenye kuweza kuleta madhara nalo ni kama bomu lililotegeshwa. Kwa kitu hafifu na kisichofaa na kudanganya vina madhara kama yalivyo madhara yanayoweza kuletwa na bomu. Hivyo basi, maana hizi nyingine katika Kiswahili zimetokana na kuchakatwa kwa nomino hiyo kwa kutumia Mchakato Sitiari wa Kisemantiki (MSK).

Kwa upande wa nomino za Kiarabu tumetumia *taharuki*. Nomino *taharuki* ilikuwa na maana nne katika Kiarabu na kubakiwa na maana mbili ilipopokewa katika Kiswahili. Maana zinazopatikana katika Kiarabu ni: 1. *Kujongea* (*kukoroga, kusogeza* au *kutikisika*), 2. *Kuwa katika mwendo au kuanza kujongea*, 3. *Kuondoka*, na 4. *Kuwa na wasiwasi au kuwa na shauku*. Katika Kiswahili neno hilo lina maana mbili ambazo ni 1. *hali ya kutokuwa na utulivu au umakini* na 2. *hali ya kusubiri, kusisimka na kuwa na hamu kujua kitakachotokea*. Maana hizi zilizomo katika Kiswahili zinaonekana kuwa zinatokana na kupachuliwa kwa maana namba 4 iliyomo katika Kiarabu. Hivyo ni maana namba 4 iliyomo katika Kiarabu ndiyo iliyoingia katika Kiswahili na kuchakatwa tena kwa kutumia MPaK na kuwa maana mbili.

### 2.1.3 Mifano ya Nomino za Mkopo Zilizopokewa kwa Kutumia MGK

Narrog (2012) anadai kuwa maana za asili za nomino au maneno kwa ujumla huweza kugeuzwa na kupatiwa maana mpya. Mchakato huu katika maneno ya mkopo umeonekana kufanya kazi zaidi katika maneno yenye asili ya Kiarabu kuliko yale ya Kiingereza. Tumetumia mifano miwili ya nomino kutoka Kiarabu kutokana na kutopatikana kwa mfano wa kufaa kutoka Kiingereza kwa ajili ya makala hii. Mifano ya nomino hizo zenye asili ya Kiarabu ni *bazazi* (بزاز) na *hawara* (خور). Nomino *bazazi* imechakatwa kwa kutumia MGK kwa kubadilishwa maana zake za asili ambazo zilikuwa zikitumika katika Kiarabu. Katika Kiarabu nomino hii inatumika ikiwa na maana za *mfanyabiashara wa nguo* na *silaha*. Nomino hiyo katika Kiswahili inatumika ikiwa na maana ya *mtu mwenye hila au mlaghai* na *mzururaji*. Maana ya *mtu mwenye hila au mlaghai* katika Kiswahili ndiyo inayotumika katika maeneo mengi ya watumia Kiswahili ilhali maana ya *mzururaji* imebainishwa na watoa taarifa kuwa inatumika Pemba tu. Nomino *bazazi* imegeuzwa maana zake zinazotumika katika Kiarabu kwa kupewa maana mpya katika Kiswahili baada ya kufananishwa mfanyabiashara wa nguo na mtu mlaghai na mzururaji. Hii imetokana na ukweli kuwa muuza nguo huwa na kauli

tamu za kumfanya mtu anunue nguo zake hivyo Waswahili wakaona kama ni mtu anayekulaghai ili ununue nguo. Vilevile, kutokana na tabia ya wauza nguo wa Kiswahili kupenda kuzunguka mtaani kutafuta wateja basi neno hilo *bazazi* likachukua dhana ya mzururaji

Mfano mwingine wa nomnio ni *hawara*. Nomino hii katika Kiarabu ina maana tatu ambazo ni: 1. *Pamba kitu*, 2. *–aliyepambwa* (*mwanamke*) na 3. *Mwanamke mwenye macho mazuri*. Maana hizi tatu zinahusiana kisemantiki kwani zote zina dhana ya kupendeza kwa kitu. Mwanamke aliyepambwa na mwanamke mwenye macho mazuri, maana zote zinaonesha uzuri wa kitu husika. Hata hivyo, neno hili lilipoingia katika Kiswahili liligeuzwa maana zake zote na kupatiwa maana mpya ambayo haina uhusiano na maana zilizomo katika Kiarabu ambayo ni *mwanamke au mwanamume anayekaa na mtu asiyeoana naye*. Kugeuzwa kwa maana ya asili na kupatikana kwa maana mpya katika lugha kopaji kunatokana na tofauti za kiutamaduni kati ya lugha kopwaji na lugha kopaji. Mathalani, utamaduni wa ndoa kati ya Mwarabu na Mswahili ulikuwa tofauti. Hivyo, Mwarabu alipokuwa akimsifia mke wake kwa kumuita hawara, Mswahili hakuithamini ndoa ile hivyo akajua neno hilo lina maana ya mtu anayeishi kinyumba.

### 2.1.4 Mifano ya Nomino za Mkopo Zilizopokewa kwa Kutumia MKK

Vilevile, zipo baadhi ya nomino ambazo zinachukuliwa na maana zake kama zilivyo. Mfano wa nomino hizo ni *ubatizo* (*baptisim*) yenye asili ya Kiingereza na *bin* ( *ابن* ) yenye asili ya Kiarabu. Nomino *ubatizo* katika Kiingereza ilikuwa na maana mbili ambazo ni *uzamishaji majini kama ishara kuwa Mkristo* na *upaji wa jina*. Nomino hii ilipokopwa na kuingizwa katika Kiswahili ilichakatwa kisemantiki kwa kutumia MKK ambapo idadi na mawanda ya maana yalibaki kama yalivyokuwa katika Kiingereza. Aidha, nomino *bin* ambayo ina maana moja katika Kiarabu, ilipokopwa katika Kiswahili iliendelea kutumika kama kwenye Kiarabu. Nomino hiyo, katika Kiarabu na Kiswahili inatumika ikiwa na maana ya *mwana wa kiume* (*wa*). Hata hivyo, imebainika kuwa nomino hii ikiungana na nomino nyingine katika Kiswahili maana hiyo hupanuliwa kimawanda. Mathalani, tunaposema bin Adam /binadamu/, yaani mwana wa Adamu huwa inabeba jinsi zote. Yaani, mwanamume na mwanamke wote ni binadamu. Hivyo, inaonekana nomino hiyo katika Kiswahili inatumika ikiwa na maana yenye mawanda mapana zaidi.

Mabadiliko ya maana yaliyotokea katika nomino hizo za mkopo mara baada ya kukopwa na kuingia katika Kiswahili yanatokana na matumizi ya nomino hizo na mahitaji ya Waswahili katika kuwasiliana kwao. Matumizi na mahitaji ya

jamii[10] ya Waswahili yamefanya maana za nomino hizo kupanuliwa, kupunguzwa, kugeuzwa au kubebwa kama zilivyokuwa katika lugha Kopaji.

## 3.0 Sababu za Upokezi Kisemantiki wa Nomino za Mkopo katika Kiswahili

Kuna sababu mbalimbali zilizosaidia nomino hizo za mkopo zipokewe kisemantiki kwa kupanuliwa, kufinywa au kugeuzwa maana zake katika Kiswahili. Kwa ajili ya makala hii tunajadili sababu kuu mbili ambazo tunaona zimechangia kwa kiasi kikubwa katika mapokezi hayo ya kisemantiki. Sababu hizo ni mahitaji ya kifahiwa na tofauti za kiutamaduni kati ya lugha kopaji na lugha kopwaji.

## 3.1 Sababu za Mahitaji ya Kifahiwa[11]

Kwa hakika kila nomino ya mkopo katika lugha kopaji ilikuwa na maana zake katika lugha kopwaji. Hivyo basi, inapopokewa katika lugha kopaji nomino hiyo huchakatwa kisemantiki kutokana na mahitaji ya kifahiwa yaliyokuwapo katika lugha kopaji. Ikitokea kuna haja ya neno hilo kuongezewa maana basi MPK hutokea, ikiwa nomino hiyo ina maana nyingi zisizohitajika katika lugha kopaji, basi maana hizo zitapunguzwa na MFK hutokea, ikiwa maana zake zinahitaji kubadilishwa kabisa, MGK hutokea na kama zinahitajika kama zilivyo, MKK hutokea. Hivyo basi, kutokana na sababu hii, Kiswahili kimechakata nomino nyingi sana zenye asili ya Kiingereza na Kiarabu.

Katika makala hii tumetumia nomino mbili kutoka katika Kiingereza na nyingine mbili kutoka Kiarabu ili kupunguza ukubwa wa makala. Mifano ya nomino kutoka Kiingereza ni *ubatizo* (baptism) na *ovataimu* (overtime) na kwa upande wa Kiarabu tumetumia nomino *ahadi* (عهد) na *idara* (إدارة). Nomino *ubatizo* ilikuwa na fahiwa mbili katika Kiingereza ambazo ni *Uzamishaji majini kama ishara kuwa Mkristo* na *–kumpa jina*. Kutokana na uhitaji wa msamiati kuelezea dhana ya ubatizaji iliyoingia katika Kiswahili, watumiaji wa Kiswahili walichakata nomino hiyo kisemantiki na kuibeba na maana zake zote na kusababisha mchakato wa MKK kutokea. Nomino nyingine yenye asili ya Kiingereza ni *ovataimu*. Nomino hii imechakatwa kisemantiki kutokana na mahitaji ya kifahiwa pia. Dhana ya kazi za kuajiriwa haikuwapo katika jamii ya Waswahili/Wabantu. Watu walikuwa wakifanya kazi yoyote kulinganana nguvu walizonazo na wakichoka hupumzika. Suala la kazi za kuajiriwa na watu kupangiwa muda wa kufanya kazi lilikuwa geni kwa Waswahili. Waingereza walikuja na neno lililokuwa na dhana ya muda wa nyongeza wa kufanya kazi kwa malipo yatokanayo na kazi hiyo ambayo ni ‘overtime’. Katika Kiingereza nomino hii hutumika ikiwa na maana tatu ambazo ni: 1. *Muda wa ziada unaofanyiwa kazi baada ya muda wa kazi*, 2. *Pesa*

---

[10] Matumizi na mahitaji ya mawasiliano ya jamii ndiyo misingi mikuu ya Nadharia ya Sarufi Amilifu iliyoasisiwa na Dik (1997).

[11] Fahiwa ni kisawe cha neno la Kiingereza ‘sense’.

*zinazopatikana kwa kufanya kazi za ziada* na 3. *Muda unaoongezwa michezoni ili mshindi apatikane*. Kutokana na Waswahili kuhitaji fahiwa za kubeba dhana hiyo ya muda wa kazi wa ziada na malipo yatokanayo na kazi hiyo walilichakata neno hilo lililokuwa na maana zipatazo tatu na kubakiza mbili katika Kiswahili ambazo ni *kazi zinazofanywa baada ya saa za kazi* na *malipo ya kazi ya ziada au ajari*. Kutokana na kupunguzwa kwa fahiwa tatu hadi mbili kumesababisha mchakato wa MFK kutokea.

Nomino *ahadi* katika Kiarabu ilikuwa na fahiwa tatu (*Ahadi*, *Ufahamu*, na *Wakati*/*kipindi*). Kutokana na mahitaji ya kifahiwa katika jamiilugha ya Waswahili neno hili lilichakatwa kisemantiki na kuchukuliwa maana zake mbili za *ahadi* na *wakati* na kuicha maana ya *ufahamu* ambayo haikuhitajika katika nomino hiyo. Kutokana na kupunguzwa kwa idadi ya maana kutoka tatu hadi mbili ni wazi kuwa MFK ulitokea. Nomino *idara* nayo pia imepokewa kisemntiki kutokana na sababu ya mahitaji ya kifahiwa. Nomino hii ina maana tatu katika Kiarabu ambazo ni 1. *Uongozi au utawala*, 2. *Kitengo au ofisi ya mipango,* 3. *Utawala ulio chini ya wizara.* Neno hilo lilichakatwa kisemantiki na kulifanya kubakiwa na maana moja katika Kiswahili ambayo ni *sehemu mojawapo ya taasisi, shirika, ofisi n.k.* Kwa vile Waswahili walihitaji fahiwa inayoelezea dhana ya sehemu katika taasisi na si utawala au uongozi kwa ujumla, iliwalazimu kulichakata neno hilo na kupunguza maana zake kutoka tatu (3) hadi moja na hivyo kusababisha MFK kutokea.

### 3.2 Sababu Zinazotokana na Tofauti za Kiutamaduni

Pamoja na nomino nyingi kuonekana kuwa uchakatwaji wake wa kisemantiki hutokana na mahitaji ya kifahiwa, bado kuna nomino nyingine ambazo zimepokewa kisemantiki kutokana na tofauti za kiutamaduni. Jamiilugha ya Waingereza, Waarabu na Waswahili zina tamaduni tofauti. Utofauti huo wa kiutamaduni kati ya lugha kopaji na lugha kopwaji umesababisha baadhi ya nomino za mkopo katika Kiswahili kuchakatwa kisemantiki. Katika data yetu ya nomino za mkopo katika Kiswahili kutoka Kiingereza na Kiarabu, kuna baadhi ya nomino zimechakatwa kutokana na lugha hizo kopwaji kutofautiana kiutamaduni. Katika sababu hii tumetumia mifano ya nomino mbili kutoka Kiingereza na mbili kutoka Kiarabu. Katika Kiingereza tumetumia nomino *gauni* (gown**)** na *goli* (goal) na katika Kiarabu tumetumia *hani* (هنّأ) na *hawara* (خور).

*Gauni* kwa utamaduni wa watumiaji wa Kiingereza linaweza kuvaliwa na mwanamke au mwanamume kulingana na shughuli ifanyikayo lakini kwa utamaduni wa watumiaji wa Kiswahili vazi hilo halivaliwi na wanaume na likabaki kuwa gauni. Hivyo basi, watumiaji wa Kiswahili kutokana na utamaduni wao wakaichakata nomino hiyo iliyokuwa na maana tatu katika Kiingereza na kubakiwa na maana moja katika Kiswahili. Maana zinazopatikana katika Kiingereza ni: 1. *Vazi la kike hasa refu litumikalo kwa wakati maalumu kama vile*

*jioni au harusini*, 2. *Joho linalovaliwa na majaji au kwenye mahafali* na 3. *Vazi refu livaliwalo juu ya lingine ili kulihifadhi la ndani hasa hospitalini*. Inayotumika katika Kiswahili ni *kanzu au vazi refu livaliwalo na wanawake*. Kutokana na kupunguzwa kwa idadi ya maana za neno 'gauni' kutoka tatu hadi moja, ni dhahiri kuwa nomino hiyo imechakatwa kwa kutumia MFK ambao umesababishwa na tofauti za kiutamaduni. Kwa upande wa nomino *goli* katika Kiingereza ilikuwa na maana nne na kutokana na tofauti za kiutamaduni ni maana mbili tu zilizoingia katika Kiswahili. Mathalani, maana ya *sehemu inayoonyesha mwisho wa mbio* haikuingia katika Kiswahili kwani kwa Waingereza mbio huishia sehemu iliyo na miamba mitatu kama lilivyo goli la mpira wa miguu lakini kwa Waswahili mwisho wa mbio huwekwa kamba tu. Hivyo basi, tamaduni tofauti zimesababisha neno hilo kuchakatwa kisemantiki na MFK kutokea.

Nomino *hani* katika Kiarabu ina maana ya kumpongeza mtu aliyefanya jambo jema, lakini kutokana na utamaduni ya Waswahili kujaliana na kuthaminiana mara baada ya mtu kupatwa na maafa, wakalibadilisha neno hilo na kuliongezea maana ya kumpa pole mtu aliyepatwa na msiba. Kwa hiyo, MGK katika neno hili umetokana na jamii hizi kuwa na tamaduni tofauti. Kwa nomino *hawara* pia imechakatwa kisemantiki kutokana na tofauti za kiutamaduni. Nomino hiyo katika Kiarabu inatumika ikiwa na maana za kupamba kitu, (mwanamke) aliyepambwa au mwanamke mwenye macho mazuri. Waarabu walipoingia pwani ya Afrika Mashariki waliwaoa wanawake wa Kiswahili na mara nyingi waliwaita kwa jina la *hawara* wakiwa na maana ya kuwasifu wake zao. Kutokana na tofauti za kiutamaduni kati ya ndoa za Waswahili na Waarabu, Waswahili hawakuichukulia ndoa ya Kiarabu kama ndoa na wakaamini dada zao wanaishi na Waarabu bila ndoa. Kutokana na hali hiyo, wakalichakata kisemantiki neno *hawara* kwa kulipa maana (*mwanamke au mwanamume anayekaa na mtu asiyeoana naye, kimada, bibi*) ambayo ina dhana tofauti na dhana iliyomo katika Kiarabu.

## 4.0 Hitimisho

Lengo la makala hii lilikuwa ni kuchunguza namna nomino za mkopo kutoka Kiingereza na Kiarabu zilivyopokewa kisemantiki katika Kiswahili. Ili kufanikisha mjadala wetu makala iliangalia kwanza namna Kiswahili kilivyokuwa na maingiliano na jamiilugha hizi. Makala imeonesha kwamba upokezi wa nomino kisemantiki huhusisha michako mbalimbali kama vile kupanuliwa maana, kupunguzwa maana, kugeuzwa maana za asili au kuchukuliwa kama zilivyotumiwa katika lugha kopwaji. Hivyo, michakato mikuu ya kisemantiki iliyotumika kupokea nomino hizo za mkopo katika Kiswahili ni MPK, MFK, MGK na MKK. Kwa kutumia mifano ya nomino kutoka Kiingereza na Kiarabu makala imeonesha kwamba sababu kubwa ya mapokezi hayo ya kisemantiki ni

mahitaji ya kifahiwa na tofauti za kiutamaduni kati ya lugha kopaji na lugha kopwaji.

## Marejeleo

Ade Ajayi, F. (1999). *Historia Kuu ya Afrika*. VI. Afrika Kwenye Karne ya Kumi na Tisa hadi

Miaka ya 1980. (Toleo lililofupishwa) Dar es Salaam: TUKI.

Baalbaki, R. (1995). *A Modern Arabic – English Dictionary* (Toleo la 7), Beirut: Dar El-Ilm Lilmalayin.

Bosha, I. (1994). *The Influence of Arabic Language on Kiswahili with Trilingual Dictionary* (*Swahili- Arabic- English*). Dar es Salaam: DUP.

Campbell, L. (2004). *Historical Linguistics: An Introduction.* Cambridge, MA: MIT Press.

Crowley, T. (1997). *An Introduction to Historical Linguistics*. (toleo la 3), New York: Oxford University Press.

Dik, S. C. (1997). *The Theory of Functional Grammar*. New York: Mouton de Gruyter.

Lodhi, A. (2000). *Oriental Influences in Swahili: A Study in Language and Cultur Contacts*, Göteborg: Acta Universitis Gothoburgensis.

Maganga, C. (2008). Maendeleo ya Matumizi ya Kiswahili Tanzania Bara. *Ukuzaji wa Istilahi za*

*Kiswahili*, Kiango, J. G (mh), Uk. 30 – 43. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B, Kihore, Y. M na Hokororo, J. I. (2001). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mohamed, M. (2010). *A Study of Adaptation of Arabic Loanwords in Swahili Dictionary: A Case of Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI 2004)*. Tasnifu ya Umahiri (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Narrog, H. (2012). *Modality, Subjectivity, and Semantic Change*: *A Cross Linguistics Perspectives*. New York: Oxford University Press.

Nurse, D na Spear, T. T. (1985). *The SWAHILI: Reconstructing the History of an African Society800 – 1500*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Oxford. (2010). *Oxford Advanced Learners' Dictionary* (Toleo la 8). New York. Oxford University Press.

Parpart, J. L na Rostgaard, M (wah) .(2006). *The Practical Imperialist: Letters from A Danish Planter in German East Africa, 1888 – 1906*. Leiden: Brill Academic Publishers.

Polomé, E.(1967). *Swahili Language Handbook*. Washington DC: Centre for Applied Linguistics.

Qafisheh, H. A. (1997). *NTC's Gulf Arabic – English Dictionary*. Chicago: NTC Publishing Group.

TUKI. (2006). *Kamusi ya Kingereza – Kiswahili* (Toleo la Tatu). Dar es Salaam: TUKI.

_____.(2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la Tatu). Nairobi: Oxford University Press

Ullmann, S. (1977). *Semantics: An Introduction to the Science of Meaning* (Toleo la 7). Oxford: Basil Blackwell.

Whitney, W. D. (1867). *Language and The Study of Language: Twelve Lectures in the Principles of Linguistic Science.* London: N. Trübner.

Zawawi, S. M. (1979). *Loan Worsd and Their Effect on The Classfication of Swahili Nominals*. Leiden: E. J. Brill.